

المجتمعي للأمن ركائز

HOTUBA YA IJUMAA.

Nguzo za Usalama wa Kijamii.

Imefasiriwa na

profesa Ayman Alasar

Shukrani zote anastahiki Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe vyote. Mwenye kusema ndani ya Kiatabu chake: {**Wale ambao wameamini, na hawakuchanganya imani yao na dhulma - hao ndio watakao pata amani na wao ndio walio ongoka**}. Ninashuhudia kuwa hakuna Mola wa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu peke yake hana mshirika. Na ninashuhudia kuwa Mtume wetu Muhammad S.A.W ni mja wake na Mtume wake. Ewe Mwenyezi Mungu peleka amani na baraka kwake Mtume pamoja na watu wa nyumbani kwake Maswahaba zake na wale wote waliowafuata kwa wema mpaka siku ya malipo.

Baada ya Utangulizi huo....

Kwa hakika neema ya usalama ni katika neema kubwa ambayo Mwenyezi Mungu Mtukufu amewapa waja wake, ambapo Anasema Mwenyezi Mungu: {**Kwa walivyo zoea Maqureishi * Kuzoea kwao safari za kifuku na kiangazi * Basi na wamuabudu Mola Mlezi wa Nyumba hii * Ambaye anawalisha wasipate njaa, na anawalinda na hofu**}. Na Anasema tena Mola Mtukufu: {**Je! Kwani Sisi hatukuwaweka imara sehemu takatifu penye amani, ambapo huletewa matunda ya kila aina kuwa ni riziki itokayo kwetu? Lakini wengi wao hawajui**}. Na Anasema tena Mwenyezi Mungu Mtukufu: {**Je! Hawaoni ya kwamba tumeifanya nchi takatifu ina amani, na hali watu wengine wananyakuliwa pembezoni zao? Je! Wanaamini upotovu, na neema za Mwenyezi Mungu wanazikataa?**}. Na anasema Mtume S.A.W: "*Miongoni mwenu mwenye kuwa na amani nyumbani kwake, mwenye afya njema mwilini mwake, ana chakula cha siku basi anakuwa kama mwenye kumiliki dunia na vilivyomo*". Yasiyokuwa na shaka ni kuwa usalama na kazi ya kijamii inayoshirikisha watu wote, ambapo hakuna yeote kati yao anayeweza kujiimarishia usalama wake mwenyewe pamoja na familia yake kwa kujitenga na usalama wa jamii, kwani watu ndani ya jamii yao na nchi yao wanafanana na abiria wa kwenye jahazi moja ambalo hawawezi kuokoka baadhi ya bila ya wengine, anasema Mtume SAW: "*Mfano wa*

watu wanaotekeleza amri za Mwenyezi Mungu na wale walioacha kutekeleza ni kama mfano wa watu waliomo kwenye jahazi, wakavutana baadhi waliopo juu na wale wengine waliopo chini, wakawa wale waliopo chini wanapotaka kunywa maji lazima wapite kwa wale walio juu yao, wakawa wanasema: Lau tutatoboa tundu ili tujipatie maji bila ya kuwakera walio juu yetu, basi ikiwa watawaacha kufanya walichotaka kufanya wataangamia wote, na kama watawazuia kwa mikono yao basi wataokoka na kuokoka wote”.

Usalama huu wa jamii una misingi na nguzo, mionganoni mwa misingi hiyo: Ni kuimarisha upande wa Kiimani ambao unaleta utulivu ndani ya jamii, na kuilinda kutokana na misimamo mikali na ukengeukaji wa kifikra, ambapo Anasema Mola Mtukufu: {**Wale ambao wameamini na nyoyo zao zikatulia kwa kumtaja Mwenyezi Mungu, fahamu kumtaja Mwenyezi Mungu kunatuliza nyoyo**}, kuamini Mwenyezi Mungu Mtukufu ndio kunaleta usalama wa ndani ya watu kwenye jamii jambo linalo akisi usalama wa jamii yote.

Miongoni pia: Ni upande wa kiuchumi ambao unsimama kwenye kufanya kazi kuzalisha na umakini, hivyo dini yetu ya kati na kati imehimiza kufanya kazi, na kuifanya kwa uzuri na kwa umakini mkubwa, ambapo Anasema Mola Mtukufu: {**Waambie wafanye kazi kwani Mwenyezi Mungu pamoja na Mtume wake na Waumini wataiona**}. Na Anasema pia Mola Mtukufu: {**Fanya vizuri kama vile Mwenyezi Mungu alivyofanya uzuri kwako, wala usilete uharibifu duniani, hakika Mwenyezi Mungu hawapendi wenyewe kufanya uharibifu**}}. Na anasema Mtume wetu Muhammad S.A.W: “*Hakika Mwenyezi Mungu anapenda pindi mmoja wenu anapofanya kazi afanye kwa umakini*”, kwa kufanya hivyo hufikiwa usalama na utulivu wa jamii.

Miongoni pia mwa misingi: Ni kuimarisha misingi ya ushirikiano na huruma ndani ya jamii, ambapo dini yetu ya kati na kati imetoe kipaombele upande huu kwa uangalifu maalum, ukalazimisha utoaji zaka na kuhimiza utoaji sadaka ukaweka Sharia ya kuhamasisha hayo, ambapo Anasema Mola wa Haki: {**Mfano wa wanaotumia mali zao katika Njia ya Mwenyezi Mungu ni kama mfano wa punje moja iliyochipuza mashuke saba. Katika kila shuke zimo punje mia. Mwenyezi Mungu humzidishia amtakaye, na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua zaidi**}}. Na Anasema tena: {**Na kheri yoyote mnayo toa ni kwa nafsi zenu. Wala msitoe ila kwa kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu. Na kheri yoyote mtakayo toa mtalipwa kwa ukamilifu, wala hamtadhulumiwa**}. Na anasema Mtume wetu Muhammad S.A.W: “*Mwenye kumuondolea Muumini tatizo katika matatizo ya dunia*.

Mwenyezi Mungu atamuondolea matatizo ya siku ya Kiyama. Mwenye kumsaidia mtu mwenye mazito Mwenyezi Mungu atamrahisishia duniani na akhera. Mwenye kumsitiri Muislamu Mwenyezi Mungu atamsitiri duniani na akhera, na Mwenyezi Mungu humsaidia mja yule mwenye kusaidia ndugu yake". Anasema tena Mtume S.A.W: "Mtu mwenye ziada ya mzigo aliyombebesha mnyama basi na amuandalie yule asiye nao. Na mwenye ziada ya maandalizi basi na amuandalie yule asiyekuwa na maandalizi" mpaka tukadhani kuwa hana haki yejote miongoni mwetu katika kilichozidi.

Miongoni mwa nguzo muhimu za usalama wa jamii ni kuimarisha msingi wa usawa kati ya watu, kwani watu wote ni sawa kama vile meno ya chanuo, na jamii yenye usalama na ustawi haina ubaguzi kati ya wananchi wake kwa misingi ya rangi au khabila, ambapo anasema Mtume wetu S.A.W: "*Enyi watu, fahamuni kuwa Mola wenu ni mmoja, na baba yenu ni mmoja, hivyo hakuna ubora kwa Muarabu dhidi ya asiyekuwa Muarabu, wala ubora wa asiyekuwa Muarabu kwa Muarabu, wala mtu mwekundu kwa mtu mweusi, wala mtu mweusi kwa mtu mwekundu isipokuwa ni ucha-Mungu*", wala hakuna ubora kwa watu wa jamii isipokuwa ni kwa msingi wa uwezo na kwa mujibu wa juhudini anazofanya mtu zinazo nufaisha jamii.

HOTUBA YA PILI:

Shukrani ni za Mwenyezi Mungu, swala na salamu zimwendee hitimisho la Manabii na Mitume naye ni Mtume wetu Muhammad S.A.W pamoja na Watu wa nyumbani kwake na Maswahaba zake wote.

Hakuna shaka kuwa kufikiwa kwa usalama wa kimazingira ni katika nguzo muhimu za usalama wa jamii, kwa kukuza mazingira na kuyalinda kutokana na madhara yejote au hatari, ambapo Anasema Mola Mtukufu: {**Yeye ndiye aliye kuumbeni katika ardhi na akakuwekeni humo**} . Na anasema Mtume S.A.W: "*Muislamu hapandi mti kisha matunda yake yakaliwa na mwanadamu au mnyama au ndege isipokuwa kwake inakuwa ni sadaka inayoendelea mpaka siku ya kiyama*". Na anasema tena Mtume S.A.W: "*Imani ina sehemu sabini – au sehemu sitini – sehemu bora zaidi ya Imani ni kusema: Laa ilaaha illa Allah "Hakuna Mola wa haki*

isipokuwa Mwenyezi Mungu” na sehemu ya chini zaidi ni kuondoa kero barabarani”.

Sisi ni wenyе kuhitaji zaidi kuunganisha juhudи kwa lengo la kufikia usalama wa jamii na kuulinda, kupitia ushirikiano wa taasisi zote za dola, kuanzia jeshi polisi mahakama familia na sekta ya elimu, taasisi za kidini kitamaduni na kiraia, ili kufikia usalama kwa watu wote ndani ya jamii kwa juhudи zao wakiwa wenyе kushirikiana.

Ewe Mwenyezi Mungu tudumishe pamoja na kudumisha nchi yetu ya Misri na nchi zengine za Waislamu neema ya usalama na amani.